# MAOMBI YA KUFUNGA

***Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na ibilisi. AKAFUNGA SIKU AROBAINI MCHANA NA USIKU, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akamjibu akasema imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."***
***[MATHAYO 4:4 ].***

***"Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na KUFUNGA, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha KUFUNGA NA KUOMBA, wakaweka mikono Yao juu Yao, wakawaacha waende zao.***
***[MATENDO 13: 2-3]***

***"Malaika wa Bwana akamwendea mara ya pili, akamgusa, akasema, inuka ule, maana safari hii ni kubwa mno kwako. Akainuka, akala, akanywa, akaenda kwa nguvu za chakula hicho siku AROBAINI MCHANA NA USIKU hata akafika HOREBU, mlima wa Mungu."***
***[1WAFALME 19: 7-8].***

**MCH. JUSTICE B. LUTASHOBYA**

# MAOMBI YA KUFUNGA

**Copyright 2014: Mchungaji Justice B.Lutashobya**

***Design by: LIBERTY MEDIA CO.LTD***
***Cell: + 255 717 599958 / 767 599958***
***Email: liberty.co12@gmail.com***

***Kimechapwa Tanzania Na:***
***Prosper Printing Company (PPC)***
***Meneja: +255-715-964536; +255-756-964536***
***Barua pepe: fadhilijuliasi@gmail.com***

*Chapa ya kwanza mwaka 2014*

*Haki zote zimehifadhiwa, Hairuhusiwi kunakili kitabu hiki kwa namna zozote bila ruhusa ya Mwandishi kwa ajili kuuza au kufanyia biashara.*

*Lakini unaruhusiwa kunakili Sehemu tu ya ujumbe katika kitabu hiki Kwa ajili ya Kushuhudia, kuhubiri na kufundisha wakristo Na wasio wakristo, kanisa lolote, shule za jumapili, shule za huduma Mikutano ya injili, semina ya neno la Mungu Na madarasa ya maombi.*

*Kwa mawasiliano zaidi,Tuandikie kwa anwani hii ifuatayo:*

*Justice na Adeline Lutashobya*
*World Miracle Mission Center*
*P.o Box 78620, Dar es salaam*

*Cell: 0754 -69 20 19, 0754-470 924, 0715- 470 924,*
*Email: pastorjustice@gmail.com au info@wmmctz.org*
*Web: www.wmmctz.org*

*Maandiko yote ni kutoka katika Biblia tafsiri ya Union version, isipokuwa kama imetajwa vinginevyo*



# SHUKRANI

Mungu wa Mbinguni, ninakushukuru katika Jina la Yesu na la Roho Mtakatifu uliyenihuisha kuandika kitabu cha **MAOMBI YA KUFUNGA**; kwa watu wako uliowaumba kwa mfano wako. Ufalme wako uje juu watu wako kupitia Neno lako lilitumwa kwao ili kuwaokoa na kuwaponya kutoka maangamizo yao. Ushuhuda wa Injili ya Yesu Kristo kwa ufunuo, ushauri , mafundisho na kumbukumbu za Roho Mtakatifu ndiyo uliyofanikisha maandalizi ya kitabu hiki katika nafasi ya kwanza. Heshima na Utukufu namrudishia BWANA WA MAJESHI KATIKA KITI CHA ENZI. Pili natoa shukrani kwa Mke wangu mpendwa Adeline Lutashobya kwa kujitolea kwake kuhakiki kitabu hiki kama mhariri, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Ahsante kwa maombi ya mapinduzi uliyofanya kuhakikisha kitabu hiki kinatoka katika uvuvio wa Roho Mtakatifu. Tatu nawashukuru shemeji yangu Anchila na watoto wangu wapendwa, Jesse, Joyous, Joyce na Namala ambao waliendelea kuiombea kazi hii ya mapinduzi, kuhakikisha inatimizwa. Mungu wa Mbinguni awafungulie Milango 12 ya mapinduzi katika maisha yenu. Nne, Namshukuru Maro Nyamate aliyetoa ushauri wa kina katika haki za kitabu hiki, pamoja na sadaka ya muda wake kuunda tovuti na barua pepe za huduma ya WMMC na BLESSING COMMUNITY. Mwisho namshukuru Robert Mwasongwe ambaye amesaidia

kutengeneza sehemu ya jarada ya kitabu hiki pamoja na kukipanga katika mfumo wa kutolewa chapa.

**NEEMA YA BWANA WETU YESU KRISTO, NA UPENDO WA MUNGU BABA, NA USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU, UWE PAMOJA NASI SOTE , SASA NA HATA MILELE. AMINA**



# YALIYOMO


SHUKRANI........................................................ iii
UTANGULIZI..................................................... vii

**SURA YA KWANZA.......................................1**
KUFUNGA NA KUOMBA......................................1
Kusudi la Maombi ya Kufunga .......................2
Kufunga ( Milango ya balaa) .........................7
Kufungua (Milango ya Baraka) ....................10
Maombi ya Kufunga...................................10
Kufungua (Baada ya maombi)......................16

**SURA YA PILI ..........................................19**
AINA ZA KUFUNGA..........................................19
Kufunga Usiku ..........................................20
Kufunga Mchana .......................................21
Mfungo kamili (Bila kula wala kunywa) .......23
Mfungo wa kunywa maji tu bila kula...........24
Mfungo wa kujiepusha na baadhi ya vyakula25
Muda wa kufunga .....................................26

**SURA YA TATU..........................................31**
MKUTANO WA MAOMBI.............................31

**SURA YA NNE ..........................................39**
MUSA ALIFUNGA NA KUOMBA ..........................39
Maandalizi ya Kuingia Hema la Maombi.......42

**SURA YA TANO ........................................45**
ESTA ALIFUNGA NA KUOMBA......................45

**SURA YA SITA.......................................... 47**
ELIYA ALIFUNGA NA KUOMBA. ......................... 47

**SURA YA SABA.......................................... 51**
YONA ALIFUNGA NA KUOMBA. ........................ 51

**SURA YA NANE .......................................... 57**
YESU ALIFUNGA NA KUOMBA. .......................... 57

**SURA YA TISA .......................................... 59**
KANISA LILIFUNGA NA KUOMBA. ...................... 59
MATENDO 4: ........................................... 60

**SURA YA KUMI .......................................... 63**
PAULO ALIFUNGA NA KUOMBA. ....................... 63
MATENDO 13: ........................................ 64
MATENDO 16: ........................................ 64
MATENDO 21 - 28 .................................... 65

**SURA YA KUMI MOJA ................................ 69**
MASHAHIDI WAWILI WA UFUNUO 11
WATAFUNGA NA KUOMBA ............................... 69

**SURA YA KUMI NA MBILI.......................... 71**
TAMATI71
1. Kufunga milango uovu;.......................... 76
2. Kufunga milango ya kuzimu ................... 77
3. Kufunga milango ya laana...................... 77
4. Kufungua milango ya Wokovu ................ 78
5. Kufunga milango ya mauti ..................... 78
6. Kufunga Kazi za shetani......................... 79
7. Kufunga ni kubeba msalaba .................. 80



# UTANGULIZI

***6.16 Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. 6.17 Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; 6.18 ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.***
***(MATHAYO 6)***

Maombi ya kufunga ni mlango wa ukristo ambao Bwana Yesu alifungua alipokuja kuja duniani katika kitabu cha Mathayo sura ya nne na Luka sura ya nne. Kufunga na kuomba ni kutangaza kikombe cha wokovu ulichokipokea kama mkristo na kufungulia baraka za wokovu kwako, kwa kanisa, taifa, kabila na lugha. Katika kitabu hiki ni hakika utajifunza mengi kuhusu njia za kufunga, na jinsi ya kufungua; kwa sababu palipo na kufunga kuna kufungua pia. Katika maombi ya kufunga kuna mambo tunayofungulia na kuna mambo tunayafunga; kuna milango tunafunga na kuna milango tunaifungua; kuna roho tunafunga na kuna roho tunafungulia; kuna kazi tunafungua na kuna kazi tunazifunga. Na hii inatupa picha kwamba tumepewa bila shaka funguo za kufunga na kufungua, maana kuna milango ya uzima na milango ya kuzimu (Mathayo 16:19).

Kufunga na kuomba ni kufunga uovu; kufunga dhambi ya woga, uzinzi, uchawi, uongo, kutamani, machukizo, kuua na kuabudu sana kama tunavyosoma katika kitabu cha ufunuo 21:8 na Isaya 58:6. Ni kufunga milango ya kuzimu isiyatoe makucha yake kulidhoofisha kanisa la Kristo; ili Neno la Mungu litimie kwamba amelijenga kanisa lake na milango ya kuzimu haitalishinda ( Mathayo 16:18). Ni kufunga milango ya laana na kufungua milango ya Baraka za kiroho na kimwili juu yako na juu ya taifa lako. Milango ya laana katika familia ni pamoja na wewe mkristo kuendelea kutambika kila mwezi na kila mwaka; na unasema YESU NI BWANA. Kufunga milango ya Upotevu na kufungulia milango ya WOKOVU .Maombi ya kufunga ni kufunga milango ya mauti na kufungua milango ya uzima.

Wachungaji (kwa maana ya Mitume, manabii, wainjilisti, Wachungaji na waliimu sawa na Waefeso 4:11); funga kazi au mradi unaokutenga na kazi ya Mungu. Funga kazi yoyote isiyompa Mungu utukufu, kazi na fedha ya aibu na iliyojaa kutu (YAKOBO 5:3). Umeitwa kuchunga kondoo, kulisha kondoo na wana kondoo (YOHANA 21). Kinyume na hapo mchungaji wangu ni ole kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Nabii Yeremia 23:1-4 na Ezekieli 34. Kuna wachungaji wameitwa kuchunga siyo tu kondoo wa zizi moja, bali hata kondoo wa mazizi mengine mengi. FUNGUA MAZIZI MENGI MCHUNGAJI! Funga roho ya woga, fungua kondoo ambao ni wagonjwa! Tembea na mkoba wa kichungaji na fimbo ya kichungaji ili uwafanyie



huduma kondoo waliopotea na walio zizini. Mchungaji lazima ujue tabia za kondoo walioko zizini na wale waliopotea; kuna tofauti jinsi wanavyolia, wanavyokula na wanavyotoa maziwa. Wale walipotea kuna wale waliorudi nyuma; lakini kuna wale pia mbao hawana mchungaji kabisa. Wale ambao hawana mchungaji yawezakana miongoni mwao ni mateka; wengine ni wachafu; wengine wamejinyea; wengine wanaharisha; wengine wana vidonda; wengine wamechoka; wengine wana utapia mlo; wengine wameshambuliwa na kupe wanahitaji dawa ya kuosha na wengine wamekonda. Wale waliopotea wanahitaji mchungaji awaonyeshe mlango wa kuingia zizini ( YOHANA 10:9); Na mlango wa kutokea wakati wa mashambulizi ya mbwa mwitu. MCHUNGAJI FUNGA MASHAMBULIZI YA MBWA MWITU DHIDI YA KONDOO! USINYWE MAZIWA YAO NA KULALA BALI UKESHE KATIKA LINDO NA UWE TAYARI KUKABILI MBWA MWITU.

Kufunga ni kubeba msalaba wa Yesu wa mateso na Injili ili kusulubisha dhambi ulimwenguni na wewe mkristo kusulubiwa kwa huo. Wafungulie wafungwa waliofungwa katika gereza la kiroho la shetani kwa kufunga na kuomba. Paulo na Sila walifunga na kuomba katika kitabu cha Matendo 16:25-26 na milango ya gereza ikafunguka. Unasema mbona mchungaji Paulo walimwomba Mungu na kusifu; napenda nikwambie ukisoma mstari wa 24 sura 16 inaonyesha walifungwa wakatupwa katika chumba cha ndani. Hii inaonyesha hawakupewa hata chakula, maana Biblia haija sema kwamba walipewa; hatahivyo ilikuwa usiku wa

manane . Kufunga na kuomba kutafungua wafungwa walioko katika gereza la dhambi na uovu. Paulo na Sila walifungwa kwa sababu ya dhambi za watu waliofungwa katika gereza la dhambi.

Mchungaji na Mwinjilisti Justice Lutashobya anaamini kwamba kutofunga na kuomba ni sawa na kutangaza uadui na Yesu Kristo. KUTOFUNGA NA KUOMBA NI KUUA ROHO ZA WATU AMBAZO ZIKO KATIKA GEREZA LA KIROHO, ZIMESHIKILIWA NA SHETANI ILI AZIPELEKE JEHANAMU. UNAWEZA KUWA ADUI WA MSALABA KWA KUTOOMBA NA KUFUNGA. Mwandishi wa Katibu hiki amefunua na amechambua silaha tatu anazotumia shetani kushambulia IMANI ya kufunga na kuomba; kwamba ni CHAKULA, FEDHA NA KITANDA. Ameonyesha jinsi shetani alivyokuja na chakula kwa Adamu wa kwanza (ADAMU NA HAWA) akamwangusha dhambini. Akaja tena kwa Adamu wa Pili, mbaye ni YESU KRISTO akashindwa katika Mathayo 4:4 kwa sababu ya kufunga na kuomba. Shetani hakuishia hapo katika agano jipya baada ya kushindwa kumshambulia Yesu Kristo aliwafuata wanafunzi wake, akamshambulia YUDA ISKARIOTE kwa fedha akafanikiwa kumshinda kwa tamaa ya fedha. Kwa undani zaidi na ujumbe kamili naomba ufuatane naye katika somo hili la kufunga na kuomba. Wakati unafunua kila ukurasa wa kitabu hiki, Roho wa Neema na maombi atakushukia na utaanza kuchukia chakula kuanzia saa 1, 3, 7, 10, 12, 24; siku 1, 3, 7, 12, 30, 40 na kuendelea, kisha utukufu wa Mungu utakufunika.



# SURA YA KWANZA

## KUFUNGA NA KUOMBA.

***Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na ibilisi. AKAFUNGA SIKU AROBAINI MCHANA NA USIKU, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akamjibu akasema imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” [MATHAYO 4:4 ].***

Kufunga na kuomba ni tendo la imani ambalo mkristo yeyote anatakiwa kuwa nalo vinginevyo hatakiwi kuwa mkristo, kwa sababu imani hii ni ya Kristo Yesu. Imani ya Kristo ni kufunga na kuomba! (MATENDO 13:1-3). Wakristo wa kwanza waliozaliwa mara ya pili pale Antiokia walifunga na kuomba, ndiyo maana walipindua ulimwengu kwa INJILI YA MIUJIZA (Waebrania 11). Kutoamini katika kufunga na kuomba ni sawa na kutoamini katika imani ya wokovu wa Yesu Kristo. Kufunga na kuomba ni ibada inayompendeza Mungu; maana hawezekani kumpendeza Mungu pasipo imani (WAEBRANIA 11:6). Silaha ya kiroho inayotumiwa sana na wanamapinduzi tangu Adamu, manabii, Kanisa la kwanza la mitume, Kanisa la sasa

na agano jipya hadi kufikia kurudi kwa Yesu na hata kipindi cha dhiki kuu ni MAOMBI YA KUFUNGA. Katika kitabu cha maombi ya tetemeko, nimechambua aina za maombi zinazoweza kuutetemesha ulimwengu wa giza katika ulimwengu wa roho na mwili. Kwa nini tunahitaji maombi ya mapinduzi? Hatima ya nchi, kabila na lugha iko mikononi mwa wanamaombi. Kanisa kamwe haliwezi kufanya mapinduzi ya roho za watu zilizoshikiliwa na ibilisi katika gereza la dhambi bila KUFUNGA NA KUOMBA. Ndiyo maana Mungu anatualika kuingia kwenye maombi haya katika mistari hii:

***" ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekeza, na KUOMBA, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.[ 2NYAKATI 7:14]***

## Kusudi la Maombi ya Kufunga

Kusudi la maombi ya kufunga ni kuhakikisha suluhisho la matatizo ya kiroho, kiuchumi, kisiasa na kijamii linapatikana. Katika sura hii naomba sasa tujue kwa nini tufikirie mapinduzi ya kiroho kwa maombi ya kufunga. Kwanza, Lazima ujue kwamba mapinduzi yanahitajika pale palipo na tatizo la kiroho au la kimwili. Mapinduzi ya mtu binafsi ndiyo yanaleta mapinduzi ya kifamilia kisha, ukoo , mtaa hata kufikia taifa na taifa nakisha dunia nzima. Mapinduzi yoyote katika nchi huanzia rohoni kwa mtu mmoja, kisha mtandao wa mapinduzi huundwa. Jaribu kufikiria huduma kubwa



za kiroho zilizoko duniani. Ukiangalia huduma ya David Yong Cho, Full Gospel of Yoido; ilianzia rohoni mwa Mchungaji David wa Korea ya kusini. Ukitazama huduma ya Assemblies of God Duniani, ilianzia kwa mtu mmoja anaitwa Charles Parham aliyeishi Kansas nchini Marekani na kufungua Chuo cha Biblia 1900. Ukizama mtandao wa huduma ya Moris Cerullo World Evangelism, ulianzia katika moyo wa Nabii na Daktari Moris Cerullo, kisha mke wake Thereza, kisha familia yake, ndiyo sasa umefanya mapinduzi nchi kwa nchi. Ukoministi ulivunjika kwa maombi ya mapinduzi katika kufunga na kuomba na neno la unabii wa Morris Cerullo. Unaweza kusoma kitabu changu cha maombi ya Mapinduzi na Kingine cha Maombi ya Tetemeko. Kwa ujumla mapinduzi yanalenga kuleta uamusho; ukombozi, uhuru, furaha na amani kwa watu wote.
Ndiyo maana Yesu alipozaliwa kama mwanamapinduzi malaika walisikika wakiimba na kusifu Mungu kwa maneno haya:

***"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe AMANI kwa watu aliowaridhia." [ LUKA2:14].***

Utakubaliana na mimi kwamba watanzania wengi karibu asilimia 95% hawana amani ya kutosha kwa sababu ya kukosa uhuru kiroho, kiuchumi na hata kisiasa. Wako wafungwa wengi katika gereza la kiroho na kiuchumi na wanamtumikia shetani asilimia 100%. Siasa za nchi hazina mpango wa kuleta mapinduzi ya amani kwa watanzania. Vita ya kiroho ni kubwa sana Tanzania, ndiyo maana utasikia watazania wengi

wanalalamika na kunungunika; maisha magumu kwa sababu ya watu wachache wanaojinufaisha katika nchi. Kiuchumi, wako watanzania hawana chakula, hawana mahala pa kulala, hawana mavazi. Nimekuwa nikipeleka nguo vijiji kwa vijiji Tanzania katika kufanya umisheni wa ndani ya nchi. Mijini pia, watanzania wanalala njaa wengi, hawana mahala pa kuishi, na wengi wanaishi kwa maisha ya taabu. Ndiyo, sikatai kwamba kuna watanzania wengine ni wavivu hasa wenyeji wa Pwani. Mimi najua watanzania wengi ni wachapa kazi, lakini hali zao siyo nzuri kimaisha. Hili hasa ndilo kusudi la maombi ya kufunga ambayo unatakiwa kuyafanya siyo kwa manunguniko, wala lawama kwa viongozi wanaohujumu nchi, wala mafisadi, bali KWA MAOMBI YA KUFUNGA. Huu ndiyo ujumbe wangu kwako katika kitabu hiki; ya kwamba inatosha kuendelea kulalamika juu ya serikali ya Jamhuri iliyowekwa na Mungu mwenyewe! Sasa Funga roho ya manunguniko kwa maombi ya kufunga!

FUNGA roho ya utumwa wa dhambi; funga roho ya umasikini; funga roho ufisadi; funga roho ya ibada za kishetani; funga roho ya ubinafsi; funga roho ya ushirikina; funga rohoya uchawi; funga roho ya uongo; funga roho ya ulevi; funga roho ya umalaya; funga roho ya ngono; funga roho ya mauaji ya kinyama; funga roho ya kumwaga damu; funga roho ya ibada za wafu; funga roho ya kuabudu majini; funga roho ya maagano ya mizimu; funga roho ya kafara katika Jina la Yesu! Amina. Unaweza kujaza vitabu na vitabu na orodha ndefu sana. Unangoja nini wakati



nimekupa silaha hii mkononi; piga kelele kwa sauti ya juu sana ukiwa umeshika mkononi kitabu hiki! Soma maombi haya na yatamke kwa nguvu na Roho Mtakatifu atawasha nafsi, mwili na roho yako kuomba kwa kuugua kusikoweza kutamkwa ( WARUMI 8:26). Unaweza kukesha kwa kufanya matamko ya ushindi kama haya ukiwa umefunga na kuomba; moto huu hauwezi kuzimika hadi hapo utakapoona nuru yako inachomoza na maadui wamefarakana na kukumbia. Biblia inasema maadui zako wataumbuka maana watakuonyesha maungo yao ( KUTOKA 23:27).

Kwa Tanzania, uaminifu ni mdogo sana hasa kwa wasioamini, ndiyo maana wengine wanaishi kwa taabu katika maisha yao. Uongo na utapeli, kwa taifa letu umekuwa tanzi kubwa kwa watanzania. Naamini hii ndiyo sababu ya kiroho inayowatesa watanzania wengi na kanisa tusipoomba maombi ya kufunga, inaweza kuwa laana katika taifa zima! Kama hujaokoka naomba umpokee Yesu awe Bwana na Mwokozi wa maisha yako. Fanya toba kwa dhambi hii, anza maisha ya kumtegemea Mungu asilimia 100%. Na hata kama umeokoka bado una kifungo hiki cha kusema uongo, fanya toba na jifunze kusema ukweli, hata kama utaonekana dhaifu, jitahidi kushuka. SOMA UFUNUO 21:8

Mungu ndiye wa kwanza kutangaza mapinduzi kupitia Roho wake; kimaandiko kuna sehemu nyingi ambazo zinaonyesha Mungu alitangaza mapinduzi ya watu wake baada ya kuishi kwa taabu na masumbufu.

Karibu kila kitabu tangu mwanzo hadi ufunuo ni kitabu cha mapinduzi kwa maombi ya kufunga. Katika Amosi 3:7 anasema kwamba Mungu hatafanya jambo lolote bila kuwafunulia watumishi wake manabii. Bwana anapokusudia kufanya jambo, mara nyingi anabadilisha maisha ya watu wake kimapinduzi. Maana yake anataka kufanya mapinduzi kama tunavyosoma katika mistari hii:

***" Amka, amka, jivike nguvu zake, Ee Sayuni; Jivike mavazi yako mazuri, Ee Yerusalemu, mji mtakatifu; Kwa maana tokea sasa hataingia ndani yako asiyetahiriwa, wala aliye najisi. Jikungute mavumbi; uondoke, Uketi, Ee Yerusalemu, Jifungue vifungo vya shingo yako, Ee binti Sayani uliyefungwa."[ ISAYA52:1-2].***

Katika mistari hii Mungu anatangaza mapinduzi kwa kanisa lake. Lakini lazima kanisa la Tanzania liamke, livunje vifungo vya uovu ndani yake. Hii ndiyo SAUMU aliyoichagua Bwana Yesu katika ISAYA58:6. Sayuni ni ishara ya kanisa; Israeli ni ishara ya kanisa. Kanisa la Tanzania Mungu anasema mapinduzi ya vifungo na mavumbi yafanyike kwanza; kabla ya kufanya mapinduzi katika nchi. Mapinduzi ya KWELI Tanzania yataanzia katika ROHO YA KANISA KWA NJIA YA KUFUNGA NA KUOMBA. Watanzania watatahiriwa; maana yake wataokoka kwa maombi ya kanisa la Tanzania, ambayo yatafanyika kwa kufunga. Hatutahitaji kupiga kelele sana za Injili iwapo tutafanya maombi ya kufunga kwa bidii kama vile vichaa wa



maombi. Maombi yangu mwaka huu Mungu ainue Mitume wa maombi; Manabii wa maombi; Wainjilisti wa Maombi; Wachungaji wa Maombi na Waalimu wa Maombi! Kwa sababu hiyo, Bwana anakuamusha mtumishi; AMKA! Tangaza mapinduzi kwa njia kufunga na kuomba kwa ajili ya Tanzania badala ya manunguniko; badala ya mihadhara ya siasa; badala ya maandamano; badala ya kupiga kelele za siasa! Kung`uta mavumbi ya kanisa, jivike nguo za maombi ya kufunga; tangaza mapinduzi kwa kufunga na kufungua! Vaa buti la mapinduzi! Vaa gwanda la mapinduzi! Vaa silaha ya maombi ya mapinduzi kwa njia ya Kufunga! Toka na uanze kufanya mapinduzi katika ulimwengu wa roho katika Jina la Yesu!

## Kufunga ( Milango ya balaa)

Neno la Kufunga maana yake ni tendo la imani au kiroho ambalo pia linaweza kudhihirika kimwili. Maana yake ni kuzuia na kuacha jambo fulani kwa sababu ya imani na Mungu wako. Kufunga kunatupa tafsiri kwamba kuna mlango au milango ambayo tunatakiwa kuifunga ili tuweze kufungua milango mingine. Mlango ni sehemu katika nyumba ya Mungu au nyumba ya kuishi iliyotengwa kwa ajili ya kuingia ndani na kutoka. Mlango unafunga na kufungua. Iko milango ya aina nyingi kulingana na vifaa; iko milango mikubwa; iko milango ya mbao, vyuma, aluminium na lulu kama tunavyosoma katika kitabu cha ufunuo 21: 21. Bado iko milango ya aina nyingi katika ujenzi wa nyumba kama mageti ya vyuma na miti. Milango pia iko inayofaa nje na ndani kulingana na hitaji la

mwenye nyumba. Mlango wa nje ni Mkuu, unatakiwa kuwa imara ili kuzuia baridi, mvua, wanyama wakali na wezi kuliko mlango wa ndani. Mlango unakuwa na sehemu za bawaba tatu au zaidi, kitasa, komeo na ufunguo. Ndiyo maana Yesu alisema nimewapa ufunguo MATH16:19. Bawaba zikipata kutu mara nyingi ni vizuri kuweka mafuta ili kulainisha mzunguko wake wa kufungua na kufunga.

Lakini ufunguo ndiyo mara nyingi unaruhusu kufunga na kufungua mlango au malango.Ufunguo ni sehemu muhimu sana katika kufunga na kufungua mambo ya kimwili na kiroho, kwa sababu kuna milango ya kiroho na kimwili pia. Mambo ya kiroho yanatumia milango ya kiroho na hivyo huhitaji UFUNGUO WA KIROHO. Roho zote zilizoko duniani hutumia milango au malango. Kama ambavyo ROHO YA WOKOVU huhupitia KWA YESU KRISTO ambaye ndiye Lango la mambo yote ya kiroho kwa watu wote, ndivyo roho zote za shetani mlango wake ni shetani. Matatizo mengi ya kiroho na kimwili yanayowapata wakristo na wasio wakristo yanao mlango unaofunguliwa kuyaruhusu yapite.

Kufunga na kuomba ni kufunga mlango wa uovu; kufunga dhambi ya woga, uzinzi, uchawi, uongo, kutamani, machukizo, kuua na kuabudu sanamu kama tunavyosoma katika kitabu cha ufunuo 21:8 na Isaya 58:6. Unapoingia katika maombi ya kufunga, funga roho zote ambazo zimeachiliwa katika siku za mwisho kama Paulo anavyozianisha katika waraka wake wa pili kwa Timotheo sura ya tatu na mstari wa



pili hadi wa sita. Fungua milango ya mbinguni kwa TOBA maana ufalme wa Mungu umekaribia (Mathayo 4:17). Ni kufunga milango ya kuzimu isiyatoe makucha yake kulidhoofisha kanisa la Kristo; ili Neno la Mungu litimie kwamba amelijenga kanisa lake na milango ya kuzimu haitalishinda (Mathayo 16:18). Iko milango ya kuzimu ndani ya familia yako; ndani ya nyumba yako; ukoo wako; mtaa wako; kitongoji chako; kijiji chako; kata yako; wilaya yako, mkoa wako; na taifa lako na bara lako. FUNGA MILANGO YA KUZIMU! HIYO NDIYO AJENDA YA SAUMU YAKO MPENDWA!!

Ni kufunga milango ya laana na kufungua milango ya Baraka za kiroho na kimwili juu yako na juu ya taifa lako. Milango ya laana katika familia ni pamoja na wewe mkristo kuendelea kutambika kila mwezi na kila mwaka; na unasema YESU NI BWANA. Biblia inasema alitajaye Jina la Bwana na auche uovu. Acha matambiko ya ukoo! Acha kula vyakula vilivyotolewa katika tambiko kwa roho za mizimu! Acha ibada na misa za wafu kila mwezi na kila mwaka! (EZEKIELI 24:15-18).Ndiyo maana magonjwa na mashambulizi ya mapepo hayaishi kwako. Ndiyo maana roho ya kuchaganyikiwa na ubumbuazi bado zinakutesa! NI LAANA ZA MAAGANO UNAYOSHIRIKI! Soma Mambo ya Walawi sura ya 18 na Kumbukumbu la Torati sura ya 28:15-68. Laana hizi zinatokana na dhambi ya kukaidi amri na Neno la Mungu. Kupendelea kujenga madhabahu za mizimu; majini na mapepo. Huu ni uasi wa amri ya kwanza na ya pili katika zile kumi kama zilivyoandikwa katika kitabu cha Kutoka 20 na

Kumbukumbu la Torati sura ya 5.

## Kufungua (Milango ya Baraka)

Kiroho kila jambo au tukio chini ya jua lina mlango wa kiroho ili lipate kufanyika, liwe baya au jema linapitia katika mlango uliofunguliwa. Bwana Yesu amekuwa mlango mkuu wa WOKOVU mbinguni, duniani na hata kuzimu. Shetani ni mlango wa dhambi na uovu. Iko milango ya dhambi inayofunguliwa na shetani halafu wakristo wanaingia. Lakini pia iko milango ambayo Mungu ametupa uwezo wa kuifungua na kufunga. Unaweza wewe mwenyewe kufungulia ushindi au kushindwa; unaweza kufungulia baraka au laana; unaweza kufungua na kufungua mlango wa wokovu au dhambi. Kimsingi tunapojadili ajenda ya kufunga lazima pia tuzungumze juu kufungua milango ya kiroho. Na tendo lolote la imani linao mlango; AMA UFUNGWE AU UFUNGULIWE.

## Maombi ya Kufunga

Maombi ya kufunga ni maombi yanayofanyika wakati mwili hauli wala kunywa, mlango wa kuonja umefungwa. Kimsingi unafanya maombi ukiwa umefunga chakula, kinywaji chochote kile, kazi zingine, shughuli zote au baadhi, dhambi, uovu wa aina yoyote. Ninaposema kufunga uovu,sisemi ukifungua unafungulia uovu kama tunavyojua baadhi ya dini isiyo ya kikristo inavyofunga uovu wakati wa saumu, ila ikifungua ni uovu juu ya uovu. Sasa huu



siyo mfungo wa maombi ninaofundisha. Ukifunga mlango wa uovu, unafungwa milele, na unafungulia utakatifu milele! Dini zingine za kikristo zinafunga tu wakati wa pasaka kila mwaka, na wana majina mengi mara kwarezima nakadhalika. Wengine wanafunga kula nyama tu kwa sababu wanakumbuka mateso ya Yesu Kristo pale msalabani. Lakini ukiwauliza imeandikwa wapi ambapo Yesu alituagiza tufunge na kuomba kwa sababu ya kukumbuka mateso yake msalabani, hawana maelezo ya kutosha kibiblia. Maana hata Yesu alipoona wanawake wakijipiga vifua na kumwombolezea, aliwaambia wasimlilie yeye bali nafsi zao na watoto wao. ( Luka 23:27-28). Mwandishi wa kitabu hiki hazungumzii habari ya kufunga kwa namna hii; Mwandishi wa kitabu hiki anazungumza juu kufunga kama inavyoelezwa katika AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA.

Mara nyingi roho yako inaungana na Roho Mtakatifu katika kuomba. Mwili unadhoofu kidogo, lakini Roho wa Mungu anatawala mwili, ili kuuisha na kuunyanyua kiroho. Unakuwa kama unamepanda boya linaloelea hewani. Boya au ndege imetengenezwa kwa vifaa ambavyo siyo vizito, ili liweze kulea. Kupaa kwenye ulimwengu wa roho ili ukifikie kiti cha enzi, unahitaji kupunguza uzito wa mwili. Bwana Yesu alisema kuna mambo mengine hayatafanyika ila kwa kufunga na kuomba (MATHAYO 17:21). Safari ya kuanza kupaa kwa ndege mara nyingi huwa ni ngumu, inapoanza kukimbia ili iweze kuruka. Unapoanza kufunga kwa maombi, shetani hutuma vipingamizi vingi kuzui

maombi haya. Siku ya kwanza inakuwa ngumu, siku ya pili ugumu hupungua kwa sababu Roho wa maombi anakuwa amekuingia; siku ya tatu ugumu unaondoka kabisa; siku ya nne unaanza kuruka kutoka chini katika ulimwengu wa roho. Unaweza kuniuliza swali kwa nini? Kwa sababu unakuwa umepokea nguvu mpya, na hivyo unaruka katika roho ya tai arukavyo juu sana kuliko ndege wengine ( ISAYA 40:31 ). Siku ya tano unakuwa hewani tayari, unaanza kusafiri juu kwa juu, unaanza kuona roho zinazotembea rohoni; unaanza kuona maadui zako laivu; siku ya sita unasogea juu zaidi na kuanza kukutana na mapepo uso kwa uso; unapigana uso kwa uso na majeshi ya mapepo. Unawaona malaika na jeshi la mbinguni linashuka kukuinua, unazungumza na malaika, unasikia maelekezo juu ajenda yako ya maombi! HALELUYAH! INATISHA KUPAA HEWANI LAKINI UNAKUTANA NA UTUKUFU WA MUNGU! Unaanza mashindano na mapepo wabaya katika ulimwengu wa roho kama Paulo anavyosema katika WAEFESO 6:12. Unapozidi zaidi ya siku 7, 14 hadi 21 unakuwa umepigana na upinzani wote wa kipepo, mkuu wa anga anaondoka baada ya kufunga na kuomba siku 21 kama tunavyosoma katika *habari hii katika kitabu cha Daniel* ***10.12 Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako. 10.13 Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi.***



KUKOSA MAOMBI YA KUFUNGA NI KUTANGAZA UADUI NA MUNGU KATIKA YESU KRISTO. NI KUTENDA DHAMBI YA MAUTI. KUTO FUNGA NA KUOMBA NI KUUA ROHO ZA WATU AMBAZO ZIKO KATIKA GEREZA LA KIROHO, ZIMESHIKILIWA NA SHETANI ILI AZIPELEKE JEHANAMU! UNAWEZA KUWA ADUI WA MSALABA KWA KUTOOMBA NA KUFUNGA. CHAKULA, FEDHA NA KITANDA NI MAADUI WAKUBWA WA MAOMBI YA KUFUNGA, KAMA HUJUI NDUGU YANGU UNAYESOMA KITABU HIKI. KUMBUKA ADAMU WA KWANZA ALIJARIBIWA KWA CHAKULA LAKINI AKAANGUKA, ADAMU WA PILI ALIJARIBIWA KWA CHAKULA AKASHINDA KWA ASILIMIA 100% KWA SABABU YA KUFUNGA NA KUOMBA. TUSOME PAMOJA LUKA 4:4 NA MATHAYO 4:4 . YUDA ALIJARIBIWA KWA FEDHA ALISHINDWA, AKAANGUKA MTEGONI KWA SABABU YA KUTOFUNGA NA KUOMBA! NDIYO MAANA BIBLIA INASEMA KUPENDA FEDHA NI CHANZO CHA MABAYA YOTE. SISEMI FEDHA NI MBAYA LAKINI UNATAKIWA KUITAWALA KWA MAOMBI NA KUFUNGA. UNATAKIWA KUITUMIA KWA MAOMBI YA KUFUNGA. FUNGA ROHO YA TAMAA, FUNGA ROHO ANASA, ZIOMBEE FEDHA WAKATI UMEFUNGA ILI ROHO MTAKATIFU ATAWALE WAKATI WA MATUMIZI!

**KITANDA** TUNACHOLALIA BAADA YA KUCHOKA KWA MUDA MREFU KINATUTENGA NA MAOMBI

YA KUFUNGA; SHETANI MARA NYINGI ANAPANDA MITEGO USIKU; UKIAMUKA UNAKUTA IMETEGWA, NI VIGUMU KUJUA MITEGO ILIYOTEGWA NI MINGAPI NA WAPI? NDIYO MTU ANALALA VIZURI LAKINI KESHO YAKE UNAKUTA AMEKUFA; MAPEPO MENGI YANATEMBEA USIKU. AJALI NYINGI ZINATOKEA USIKU. MAOVU MENGI YANAFANYIKA VITANDANI KATIKA MAKASINO, HOTELINI, NYUMBA ZA KULALA WAGENI NAKADHALIKA. FUNGA ROHO ZA UVAMIZI WAKATI WA USIKU, TENGA MUDA WA KUFUNGA NA KUOMBA NYAKATI ZA USIKU WA MANANE. JIFUNZE KUFUNGA USIKU, ILI UOMBE USIKU KUCHA ILI ROHO ZA MAPEPO YANAYOKUTAFUTA WAKATI UMELALA YAPIGWE NA MIALE YA MOTO INAYOTOKANA NA KUFUNGA NA KUOMBA. FUNGULIA ROHO YA MAOMBI WAKATI WA USIKU. KUNA SIRI NZITO YA KUFANYA MAOMBI YA KUFUNGA USIKU. KUMBUKA KANISA LA JANGWANI (WANA WA ISRAELI WALIKOMBOLEWA USIKU, SAFARI YAO YA UKOMBOZI ILIFANYIKA USIKU). KUMBUKA PIA YESU KRISTO ALIZALIWA USIKU NA ALIFUFUKA USIKU.

KUMFUATA KRISTO NI KUFUATA NGUZO YAKE YA MAOMBI NA KUFUNGA. ALIOMBA MPAKA MACHOZI YA DAMU. ALIFUNGA NA KUOMBA HATA PALE MSALABANI KWA SABABU BIBLIA INASEMA ALIONA KIU (YOHANA 19:28). HATAHIVYO WAKATI ANASULUBIWA HAKUNA AMBAPO TUONA ANAPEWA NAFASI YA KULA WALA KUNYWA. KATIKA MATESO YOTE MSALABANI ALIFUNGA UKISOMA MATENDO 10, UTAGUNDUA KUWA MUNGU ATAKULETEA WOKOVU



UKIENDELEA NA SALA BILA KUJALI UMEOKOKA AU HUJAOKOKA, BILA KUJALI UNATENDA DHAMBI AU HAUTENDI DHAMBI!!!

**TOKA SAA HII ANZA KUOMBA!!** MAANA SAA INAYOFUATA SHETANI ANAKUTAFUTA APATE KUKUMEZA!! HATA KAMA UNAENDESHA, HATA KAMA UKO KAZINI, HATA KAMA UKO KWENYE FOLENI, HATA KAMA UKO KWENYE MSIBA, HATA KAMA UKO HOTELINI, HATA KAMA UKO KWENYE NDEGE, HATA KAMA UNAFANYA DHAMBI, HATA KAMA UNAWAZA DHAMBI, HATA KAMA UNA MATATIZO, HATA KAMA UKO GEREZANI, HATA KAMA UKO KATIKA HALI MBAYA YA KUFA, HATA KAMA UKO KWENYE PRESHA YA KAZI, HATA KAMA HUJAPATA UNACHOKISUBIRI KWA MUDA MREFU!! OMBA TENA, ENDELEA KUOMBA, PAZA SAUTI YAKO, MPINGE SHETANI, LALAMA MBELE ZA BWANA. UMEVAMIWA WEWE, HUJUI! WATOTO NI MATEKA, MKE WAKO NI MATEKA, MUME WAKO NI MATEKA, BABA YAKO NI MATEKA, MAMA YAKO NI MATEKA, MJOMBA WAKO NI MATEKA, KANISA LAKO NI MATEKA, TAIFA LAKO NI MATEKA, UCHUMI WAKO NI MATEKA, WIZARA YAKO NI MATEKA, HUDUMA YAKO NI MATEKA, OFISI YAKO NI MATEKA, BIASHARA YAKO NI MATEKA, SHAMBA LAKO NI MATEKA, NGOMBE WAKO NI MATEKA, MAZAO YAKO NI MATEKA, NYUMBA YAKO NI MATEKA, TAALUMA YAKO NI MATEKA, FEDHA YAKO NI MATEKA! UMEIBIWA TAYARI! PIGA KELELE ZA MAOMBOLEZO! OMBA MUNGU AKUSAMEHE. OMBA MUNGU AKUFUNGUE KUTOKA KATIKA VIFUNGO VYA UCHAWI, UMASIKINI, MAGONJWA, MASHAMBULIZI

YA KIPEPO KATIKA JINA LA YESU WA NAZARETI!!!

## Kufungua (Baada ya maombi)

Nimetangulia kusema palipo na kufunga na lazima kuna kufungua, kwa sababu pia kuna mlango. Kuna majaribu mengi yametokea katika mwili wa Kristo wakati wa kufungua saumu. Kuna wapendwa ambao kwa sababu ya njaa ya tamaa ya chakula wamefanya wakristo wengine wachukie kufunga na kuomba kwa sababu ya mabaya yaliyowapata baada ya kufungua saumu zao. Napenda ujue wewe ambaye umepata neema ya kushika kitabu hiki mkononi na macho yako yana uwezo wa kusoma herufi, ya kwamba milango inapofunguliwa hasa ya maisha yako, ni Baraka. Mungu amekubariki kwa kufunga na kuomba, ili ufunguliwe milango. Sasa tunategemea na wewe unapofungua baada ya maombi upate Baraka badala ya balaa. Zuia roho ya ulafi na tamaa ya chakula ambayo hujiiuzulisha wakati wa kufungua saumu yako.

Kimsingi kufungua saumu ni sawa na kufunga saumu; kwa maana siku za kufunga zinatakiwa kuwa sawa na siku za kufungua saumu. Kama umefunga siku 3 kavu unatakiwa kuchukua siku 3 za kufungua saumu. Siku ya kwanza; kama ulikuwa hutumii maji basi nakushauri uchukue maji ya uvuguvugu yaliyochemshwa uanze kunywa kwa masaa 3, kisha unywe tena saa1, baada ya hapo unaweza kutumia vyakula vya majimaji kama juisi ya matunda au matunda au uji laini na hata supu ya moto au maziwa ya moto; hii ni siku ya kwanza ya kufungua saumu itakuwa imeisha. Siku ya pili,



unaweza kuendelea kutumia Maji asubuhi na baadaye vyakula laini vya maji maji; wakati umefungua unatakiwa kunywa maji mara baada ya saa 1. Siku ya tatu unaweza kutumia ndizi, viazi, matunda au juisi na kuendelea kutumia maji kila mara; lakini chakula utakula kidogo. Kama ulikuwa unakula sahani ya wali sasa utatumia robo au nusu ya sahani. Siku ya nne unaweza kuendelea na utaratibu wa kawaida wa kula chakula, lakini unashauriwa unywe maji wakati.

Kufungua saumu vibaya ni kula vyakula vigumu siku ya kwanza na kula bila kiasi kwa tamaa ya njaa. Mwili hukataa na unaweza kusababisha madhara katika mwili, unaweza kutapika na kuharisha vibaya. Kamwe usifungulie saumu yako kwa maziwa ya mtindi wala wali, wala ugali wala chai ya majani, wala kahawa, wala vyakula vya baridi. Bora siku ya kwanza ukafungua kwa kutumia maziwa ya moto au maji moto. Kipindi ambacho unafungua saumu, wakati wa kula sema tena na Mungu; Mwambie wakati nafungulia kula, basi nafungulia milango ya mbinguni; nafungua milango ya Baraka; nafungulia milango ya huduma, nafungulia amani, nafungulia uponyaji, nafungulia roho ya imani, nafungulia roho ya miujiza, nafungulia roho ya maombi, nagungulia roho ya unabii, nafungulia upako, nafungulia ushindi. AMINA! Mapepo kuzimu yanalia! Usinyamaze wakati unakula, mkaribishe Roho Mtakatifu wakati wa kufungua saumu, mshukuru kwa kukuongoza katika maombi ya kufunga na mshukuru kwa kukutia nguvu na kukuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa (WARUMI 8:26). Mwambie

Yesu nakukaribisha katika chakula hiki sawa na neno lako katika Ufunuo 3.20 ***Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.***